

Azimio

Tunatambua kuwa mifumo yetu chakula ya sasa inachanngia sana kwenye majanga yanayoendelea ya kiafya, mabadiliko ya tabia ya nchi, bayoanuai na uvunjifu wa haki za binadamu. Tutaweza tu kufanikisha Malengo ya Umoja wa Mataifa ya Maendeleo Endelevu kwa kufanya matengenezo makubwa katika mifumo yetu ya chakula.

Kipindi ambapo sisi kama vijana tumekuwa hatushirikishwi katika michakato ya vyombo vya maamuzi katika masuala ya msingi kisiasa na kiuchumi, japokuwa sisi ndio tutakaoishi muda mrefu tukiathiriwa na matokeo ya maamuzi yanayofanyika leo.

Tunaazimia kuchukua hatua. Tunahitaji uharaka mkubwa wa kuchukua hatua kutoka kwa wengine, hasa kutoka kwa wafanya maamuzi katika serikali na biashara. Kama vijana #ChukuahatuakwaChakula #ChukuahatuakwaMabadiliko kuwezesha #ChakulaBorakwaWote

